SISI NI NANA?

Kundi letu ni la watu wanaoishi sehemu ambazo ni jirani ya uwanja wa ndege wa Gatwick.

Tunahusika katika kuwashughurikia wale wote waliotiwa Kizuizini hapa Gatwick.

Tumejitolea kuifanya shughuri hii kwa hiari. Hatulipwi wala hatukuajiliwa na yeyote yule; bali twajimiliki.

Twatumia muda wetu katika kuwafajiri na kutoa misasda mbalimbali kuwasaidia wale waliozuiliwa hapa Gatwick wakiwa Tinsley House.

Tuko huru kabisa! Twajitegemea. Hatuubanwi wala hatukuajiliwa na madaraka ya Uhamiaji, wala Ofisi ya wale wanaohusika na madaraka ya Ulinzi wa kambi hii.

Katika kundi letu wamo walio Wakristo Waislamu, na wengineo wa Madhebehu mbali mbali, hata wale wa Madhehebu ya Kijadi pia ni wanachama.

NI NANI TUNAOWASAIDIA?

Twamsaidia ye yote yule. Hatuna ubaguzi wa rangi, wa Utaifa au Udini, wala Ukabila Ni ye yote yule anayetuomba msaada tunamsaidia.

SHUGHURI TUNAZOZIFANYA

Tunao mpango maalum; Kwani tunayo orodha rasmi, ambayo mtu wa kundi letu huweza kufanya ziara hiyo ikiwa mara moja kila wiki. Mpango huu huendelea hivyo, mpaka yule aliyewekwa kizuizini aidha ahamishwe, kupelekwa mahali pengine, au aachiliwe kwenda huru –

Hivyo basi twajaribu kujenga na kuimarisha uhusiano mwema kutokana na ziara hizi kwani twaamini kuwa ‘Akiwepo mwanadamu mwenzio munayeweza kuzungumziana na kupeana taarifa, mnaweza kushauriana na kuweza kupunguza uzito wa mawazo yaliyokuzidia tangu uwekwe humu kizuizini’. Yabidi uelewe kwamba yote hayo munayo ya zumgumzia yatasikilizwa kwa makini. Na kundi letu liko tayari kutoa msaada kiasi kinachowezekana ili kukusaidia.

Hayo yote munayoyazungumzia yanasetiliwa. Ni yenu tu na mgeni wako – Kadhalika, tunaweza kusaidia kwa mambo mengine madogodogo, kwa mfano Karatasi za Msalani, Sabuni marashi ya kuogea, Vifaa vya kujipodoa kwa wanawake, Mafuta Ya kujipaka n.k. Kwani hivi havitolewi na madaraka ya Uzuizi. Wanaolinda Kambi hii ya Gatwick. Vilevile twasaidia na nguo za mitumba. Hizi zitasaidia iwapo zile ulizokuja nazoumevaa zimechafuka. Hapa twasisitiza, tukikumbusha kwamba iwapo ukipungukiwa kama na vifaa tulivyovitaja hapo juu, usikose, kumwalifu huyo mgeni anayekutembelea. Au utupigie simu. Nambari yetu ikiwa – 01293 434 350.

Pia twaweza kukusaidia uweze kuwasilianan a na wakili anayeshughulikia kesi yako awaombe waharakishe maombi yako, yaweze kujadiliwa mapema iwezekanavyo, kwani mgeni wako ataweza kuwasiliana na huyo wakili. Walakini hii itategemea kama ukiruhusu wawasiliane naye.

Tunayo orodha ya mawakili stadi, hodari wanaoweza kuwakilisha maombi yako mahakamani. Wewe tualifu tu, tutawatafuta kwa niaba yako, mapema iwezekanavyo.

MAMBO TUSIYOWEZA KUTATIMIZA

Hatuna madaraka wala mamlaka ye yote ya kukutoa humu kizuizini.

Hatuwezi, wala hatuna kauli ya kuzuia usirudishwe nchi uliyotokea iwapo imeamriwa urudishwe huko. Sisi sio Wanasheria, na wala hatuchukui nafasi ya Uwakili. Hivyo basi hatuwezi kutoa ushauri wo wote unaohusiana na maombi yako ya kutafuta kibali cha kuishi nchi hii kama Mkimbizi.

Hatuna nguvu ye yote ya kuingilia kesi yako. Bali tuko bega kwabega, tukiwa pamoja nawe muda wote ambao maombi yako yanapojadiliwa mahakamani.

Wanachama wetu, yaani wale wanaokutembelea, hawaruhusiwi, na ni marufuku kwao kukuwekea dhamana. Hawawezi kufanya hivyo! Walakini ukitaka

kuwekewa dhamana tuma maombi yako kwa:

BID Anuani Tel 020 7247 3590
Fax 020 7247 3550

Ofisi yao iko wazi tangu saa saba u nusu mpaka saa kumi u nusu mchana kila siku.

HAKI ZAKO KATIKA TINSLEY

Katika jumba la tinsley una haki na matarajio kulingana na sheria za kituo, Ambazo ni muhimu zielezwe kwako kama itabidi uishi kwa muda mrefu.

JINSI YA KUKABILI MATATIZO

Ni sharti ujulishwe jinsi ya kukabili matatizo. Shida yako itachunguzwa na watu wasiopendelea upande wowote na hili jambo halitadhulu hali ya kesi au maisha yako katika jumba la Tinsley.

Ni sharti upatiwe mswaki na dawa ya meno, sabuni ya kuogea, shampoo, cream cha kunyolea ndevu, na vifaa vya kujipanguza bila malipo yoyote.

KAMA UMEPUNGUKIWA NA PESA

Kama una pesa kiasi ya chini ya £25, unaweza kuomba kadi ya kupigia simu ya dhamani ya £2 kutoka kwa ofisi kila wiki. Hii ni muhimu ili uweze kuasiliana na wakili wako (kwa mfano, kama unahamishwa). Au ungetaka kujitafutia wakili mwingine unaweza pia kupewa makaratasi au stamps bila malipo.

RIPOTI ZA UHAMIAJI

Kama umezuiliwa, ni lazima upatiwe ripoti yako kila mwezi, ukielezwa sababu yakuendelea kuzuiliwa kwako. Kama sio hivyo basi wasiliana na ofisi ya uhamiaji hapa Tinsley na watakusaidia kuipata.

GDWG OFFICE:

225 Three Bridges Road,
Crawley, West Sussex, RH10 1LG
Tel: (01293) 434350. Fax: (01293) 434351

FREEPHONE – 0800 389 4367

Monday - Friday 9.30am - 5.30pm

If we are not able to take your call, leave a message on the answer phone. Spell your name slowly and we will phone you back as soon as we can.

SHIRIKA LA KUSAIDIA WALIOZUIL WA GATWICK

Registered Charity No. 1053730



INFORMATION FOR DETAINEES

Swahili